
JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
HALMASHAURI YA MJI WA BABATI
HALMASHAURI YA MJI BABATI TOWN COUNCIL
MAFANIKIO YA SERIKALI YA AWAMU YA SITA KWA KIPINDI CHA MIAKA MITATU (2021-2023)
"KITABU CHA MWANANCHI"
BAJETI NA KIASI KILICHOPOKELEWA - ELIMU BILA MALIPO 2021-2024
400,000,000.00
300,000,000.00
200,000,000.00

## DIBAJI

Halmashauri ya Mji wa Babati kwa kushirikiana na wananchi na wadau mbalimbali wa maendeleo imepata mafanikio makubwa katika utendaji kazi kwa kutoa huduma bora kwa wananchi.

Katika kipindi cha miaka mitatu (3) iliyopita, tunaona mafanikio makubwa yaliyopatikana chini ya Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na **Mhe.Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**. Mafanikio haya yanaonekana katika sekta za kijamii zinazomgusa mwananchi moja kwa moja katika huduma za Elimu, Afya na Maji.

Serikali ya Awamu ya Sita imehakikisha upatikanaji wa rasilimali fedha za kuimarisha, kuboresha na kuongeza miundombinu katika utoaji wa elimu iliyo bora na huduma za Afya za kisasa kabisa.

Kitabu hiki kinaelezea mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha miaka 3 ya utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi chini ya uongozi thabiti wa Mhe. Dkt Samia Suluh Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi Taifa. Hiki ni kitabu cha mwananchi ambapo kila mwananchi atapata fursa ya kuona kazi mbalimbali zinazofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita. Kwa niaba ya Baraza la Madiwani, ninaomba kuwahakikishia wananchi wote kwamba tutandelea kusimamia ipasavyo miradi ya maendeleo inayotekelezwa katika maeneo yote ya Halmashauri yetu kwa kushirikiana na wadau wote ili kuhakikisha maendeleo endelevu ya wananchi wote.

Karibuni sana.



Abdulrahman Hussein Kololi
**Mwenyekiti**
**Halmashauri ya Mji Babati**

## DIBAJI

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imekuwa katika juhudi mbalimbali za kuhakikisha utoaji wa huduma bora kwa maendeleo ya wananchi wake ikiwa ni pamoja na uwekaji wa mazingira wezeshi ya kufanya kazi na kujipatia maendeleo endelevu.

Utoaji wa huduma bora kwa wananchi, hususani Elimu, Afya na Maji imekuwa ni kipaumbele cha Serikali ya Awamu ya Sita tokea ilipoingia madarakani mnamo mwezi Machi, 2021. Mafanikio katika miundombinu mbalimbali ya barabara na umeme yanaonekana kwa uwazi kabisa.

Halmashauri ya Mji wa Babati inajivunia mafanikio mbalimbali yaliyopatikana kutokana na uongozi thabiti wa Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**. Ni dhahiri kwamba, Serikali inao wajibu wa kuhakikisha kwamba Mwananchi anafahamishwa ipasavyo juu ya mafanikio yaliyofikiwa katika utoaji wa huduma bora kwa wananchi hususan huduma za Elimu, Afya, Maji, Barabara na Nishati licha ya changamoto ndogondogo ambazo zimekuwa zikipatiwa ufumbuzi siku hadi siku.

Katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita, Halmashauri ya Mji wa Babati pamoja na baadhi ya Taasisi zinazotoa huduma moja kwa moja kwa mwananchi zimepokelewa fedha kiasi cha **shilingi 43,541,221,720.43** ambapo Halmashauri ya Mji Babati imepokea kiasi cha **shilingi 20,218,094,665.07** zilizowezesha utekelezaji wa shughuli katika sekta mbalimbali hususan za Elimu na Afya. Utoaji wa huduma bora za afya umeimarishwa sambamba na uimarishaji wa miundombinu na utoaji wa huduma bora za elimu katika maeneo yote.

Kupitia Taasisi zinazotoa huduma kwa wananchi wa Halmashauri ya Mji wa Babati, tunaona kuimarishwa kwa huduma bora za upatikanaji wa maji safi na salama na kuboreshwa kwa miundombinu ya Barabara ambapo kiasi cha **shilingi 23,323,127,055.36** kimetolewa na Serikali ya Awamu ya Sita.

Kitabu hiki kinalenga kumfahamisha mwananchi juu ya kazi kubwa inayofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita tokea ilipoingia madarakani mwezi Machi, 2021 hadi sasa. Nawakaribisha kusoma kitabu hiki na kuendelea kuunga mkono juhudi za Serikali katika kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora kwa wananchi wote.





Pendo E. Mangali,

**Mkurugenzi, Halmashauri ya Mji Babati**

# MAFANIKIO YA SERIKALI YA AWAMU YA SITA KWA KIPINDI CHA MIAKA MITATU (2021-2023)

## 1.0 UTANGULIZI

Halmashauri ya Mji Babati ni moja ya Halmashauri saba (7) za Mkoa wa Manyara yenye ukubwa wa kilometa za mraba 472.49. Kiutawala Halmashauri ina Tarafa **2,** Kata nane **8,** Vijiji **13,** Mitaa **35** na Vitongoji **54**. Halmashauri hii ilianzishwa tarehe 17 Septemba 2004 kwa Tangazo la Serikali **Na. 352** ikimegwa toka Halmashauri ya Wilaya ya Babati.

Idadi ya watu kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022, Halmashauri ina jumla ya **wakazi 129,572** (Wanaume **65,114** na Wanawake **64,458**) sawa na asilimia 6.8 ya wakazi wa Mkoa wa Manyara.

**Shughuli za Kiuchumi katika Halmashauri ya Mji wa Babati**

Kipato cha wananchi wengi kinatokana na shughuli za Kilimo, Biashara ya mazao, Mifugo, Uvuvi, Biashara, Viwandani na Ajira.

Halmashauri ya Mji wa Babati imefanikiwa kutekeleza miradi ambayo inagusa moja kwa moja maisha ya Mtanzania. Hii ni kwa sababu "***Serikali Imewasikia Wananchi na Vilio vyao na Sasa Imewafikia kwa Kutatua Kero Zao".***

## 2.0 UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KATIKA SEKTA ZILIZOKO KWENYE HALMASHAURI YA MJI WA BABATI

Katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya 6 Halmashauri ya Mji wa Babati imepokea jumla ya **shilingi 20,218,094,665.07** kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwemo miradi ya:-

### 2.1 Sekta ya Elimu

Katika kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora za elimu na hatimaye kuweza kujishughulisha na kazi maendeleo,

***Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 - 2025*** inaelekeza katika Ibara ya 80 kwamba *"Chama katika miaka mitano ijayo, kinalenga kuimarisha ubora wa elimu katika ngazi zote kwa kuzingatia falsafa ya kujitegemea yenye kuendana na mazingira ya nchi yetu, hususan elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi".*

Katika Kipindi cha miaka 3, Halmashauri ya Mji wa Babati imepokea jumla ya **shilingi 10,681,037,531.00** kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo katika Shule za Msingi na Sekondari. Kutokana na fedha hizo Halmashauri imepata mafanikio mbalimbali katika Sekta ya Elimu kama ifuatavyo:-

### a) Elimu ya Awali na Msingi

Halmashauri imepokea jumla ya **shilingi 5,181,757,503.00** kati ya fedha hizo **shilingi 1,287,000,000.00** zilitumika kutekeleza miradi ya maendeleo na **shilingi 3,894,757,503.00** zimetumika kuboresha mazingira ya ufundishaji na kujifunzia katika Elimu ya Awali na Msingi (Elimu bila malipo na *Capitation*). Kutokana na fedha hizo Halmashauri imefanikiwa yafuatayo:-

i. Kuandikisha wanafunzi Darasa la Awali 10,768 mwaka 2021 hadi mwaka 2023 sawa na asilimia **102** ya lengo la kuandikisha wanafunzi 10,520.



***Madarasa ya awali shule ya msingi Hangoni 2023***

ii. Kuandikisha wanafunzi wa Darasa la Kwanza 11,061 mwaka hadi mwaka 2023 sawa na asilimia **103** ya lengo la kuandikisha wanafunzi 10,724.

***''Uandikishaji huu umeongeza fursa kwa watoto wengi zaidi kupata Elimu ya Awali na Msingi''.***

iii. Kuongeza idadi ya vyumba vya madarasa kutoka vyumba **306** mwaka 2021 hadi vyumba **384** mwaka 2023 sawa na ongezeko la vyumba 78 pamoja na Ofisi za Walimu 20.



***Vyumba vya madarasa shule ya Msingi Hangoni, 2023***



iv. Kuongeza idadi ya matundu ya Vyoo kutoka matundu **470** mwaka 2021 hadi matundu **591** mwaka 2023 sawa na ongezeko la matundu 121.



***Matundu 3 ya vyoo shule ya Msingi Komoto, 2023 shilingi 6,300,000.00***

v. Kuongeza idadi ya Madawati kutoka Madawati **6,120** mwaka 2021 hadi madawati **6,650** mwaka 2023 sawa na ongezeko la madawati 530.



vi. Ujenzi wa Nyumba **2** za Walimu za familia mbili (2:1) katika Shule za Msingi Kiongozi na Bambay kwa gharama ya shilingi 110,000,000.00.



*Nyumba ya walim S/M Bambay, 2023*



*Nyumba ya walim S/M Kiongozi, 2023*

vii. Kuongezeka kwa Shule za Awali na Msingi kutoka shule 27 mwaka 2020 hadi shule 34 mwaka 2023.




***Shule mpya ya msingi Queen Sendiga (2023) – shilingi 328,500,000.00***

viii. Kuboreshwa kwa mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji kupitia ruzuku ya Elimu bila malipo kugharamia uendeshaji wa Shule, chakula cha wanafunzi wa elimu maalum na posho ya madaraka kwa walimu wakuu wa shule za msingi.

Katika utekelezaji wa elimu bila malipo kiasi cha shilingi 870,508,120.67 kimetolewa na Serikali ya awamu ya Sita kama ifuatavyo;

| NA | MWAKA | BAJETI | KIASI KILICHOTOLEWA |
|---|---|---|---|
| 1 | 2021 | 211,489,593.00 | 211,485,592.96 |
| 2 | 2022 | 230,876,474.00 | 219,713,763.79 |
| 3 | 2023 | 239,451,000.00 | 263,585,258.35 |
| 4 | 2024 | 354,889,237.00 | 175,723,505.57 |
| | **JUMLA** | **1,036,706,304** | **870,508,120.67** |




**''Ongezeko la Miundombinu hii imesaidia kuboresha Elimu na kupunguza msongamano wa wanafunzi Madarasani na kutoa fursa ya walimu kufundisha katika mazingira bora na rafiki pamoja na kuongeza wigo kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum kufikiwa kwa urahisi''.**

**''Vilevile imeimarisha usalama wa watoto pamoja na kupunguza utoro''.**

ix. Kuongezeka kwa ufaulu wa wanafunzi katika mitihani ya kumaliza Darasa la Nne kutoka 87% mwaka 2021 hadi kufikia 96.5% mwaka 2023.

x. Kuongezeka kwa ufaulu wa wanafunzi katika mitihani ya kumaliza Darasa la Saba kutoka **86%** mwaka 2019 hadi kufikia **91.7%** mwaka 2023.



## b) Elimu ya Sekondari

***Ibara ya 80(a)***

*"Kuendeleza mpango wa kutoa elimu bila malipo kwa shule za sekondari ili kuwawezesha vijana wenye sifa kuanza na kuendelea na masomo bila kikwazo".*

Katika kipindi cha mwaka 2021 – 2023, Halmashauri imepokea kiasi cha **shilingi 5,499,280,028.00** kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo katika Sekta ya Elimu Sekondari. Kutokana na fedha hizo Halmashauri imepata mafanikio kama ifuatavyo:-

i. Kuongezeka kwa wanafunzi waliandikishwa kujiunga na Kidato cha Kwanza kutoka wanafunzi **2,084** mwaka 2021 hadi wanafunzi **2,301** mwaka 2023.

ii. Kuongeza kwa idadi ya vyumba vya Madarasa kutoka Vyumba **223** mwaka 2021 hadi Madarasa **250** mwaka 2023.



*Picha: Madarasa 4 Shule ya sekondari Gekul, 2022, Shilingi 80,000,000.00*

iii. Kuongeza idadi ya Matundu ya vyoo kutoka Matundu **149** mwaka 2021 hadi Matundu **215** mwaka 2023.



Choo shule ya wasichana kata ya Maisaka, 2024

iv. Kuongeza idadi ya Maktaba kutoka **2** mwaka 2021 hadi **4** mwaka 2023.





*Maktaba shule ya Sekondari Sigino, 2023 – Shilingi 92,387,000.00*

v. Kuongezeka kwa Idadi ya Vyumba vya Maabara kutoka vyumba **36** mwaka 2021 hadi Vyumba vya Maabara **42** mwaka 2023.



***Maabara shule ya Sekondari Hangoni, 2022***

vi. Kuongezeka kwa idadi ya Nyumba za Walimu kutoka **18** mwaka 2021 hadi nyumba **20** mwaka 2023.



*Nyumba ya mwalimu, (2in1) Gekul Sekondari.*

vii. Kuongezeka kwa shule za Sekondari, kutoka shule 14 mwaka 2021 kufikia shule 16 mwaka 2023.



*Baadhi ya vyumba vya madarasa shule mpya ya Sekondari, Kololi, 2024*

viii. Kuanzishwa kwa **Shule mpya ya Sekondari ya Wasichana** ya Mkoa kwa gharama ya shilingi 3,000,000,000.00




*Jengo la Utawala shule ya Wasichana ya Mkoa wa Manyara, 2024*




*Vyumba vya madarasa shule ya Wasichana ya Mkoa wa Manyara, 2024*

ix. Kuboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji kupitia ruzuku ya elimu bila malipo ambapo jumla ya **shilingi 1,056,763,901.37** zimepokelewa kwa ajili kugharamia uendeshaji wa Shule, Chakula cha wanafunzi wa Kidato cha Tano na Sita, Fidia ya Ada na posho za Madaraka kwa wakuu wa Shule za Sekondari na Maafisa Elimu wa Kata.


| NA | MWAKA | BAJETI | FEDHA TOLEWA |
|---|---|---|---|
| 1 | 2021 | 286,022,500.00 | 229,519,597.00 |
| 2 | 2022 | 265,845,000.00 | 247,472,083.12 |
| 3 | 2023 | 347,863,332.75 | 347,863,332.75 |
| 4 | 2024 | 349,286,043.00 | 231,908,888.50 |
| **JUMLA** | | **1,249,016,875.75** | **1,056,763,901.37** |




x. Kuimarika kwa ufaulu wa wanafunzi katika Mitihani ya Kidato cha Nne kutoka **98%** mwaka 2019 hadi kufikia **99%** mwaka 2023.




xi. Kuendelea kuimarika kwa ufaulu wa wanafunzi katika Mitihani ya kumaliza Kidato cha Sita kwa **asilimia 100** kwa miaka 3 (2021 hadi 2023).




xii. Kuongezeka kwa idadi ya Viti na Meza za wanafunzi kutoka Viti 5,142 mwaka 2021 hadi Viti 7,173 mwaka 2023.



*Meza na viti shule ya Sekondari Kololi, 2024*

## 2.2 Sekta ya Afya

***Ibara ya 83 ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM (2020)***

*"Lengo la Chama ni kuhakikisha wananchi wanakuwa na afya na siha bora ili kuwawezesha kushiriki katika shughulli za ujenzi wa Taifa na kuboresha maisha yao".*

Halmashauri imeendelea kuimarisha, kuboresha na kujenga Vituo vya kutolea Huduma za Afya ambapo jumla ya **shilingi 6,695,655,831/=** zimepokelewa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo na utoaji wa huduma za afya. Kabla ya Serikali ya Awamu ya 6, Halmashauri ilikuwa na Vituo vya kutolea Huduma 8 (Hospitali 1, Kituo cha Afya 1 na Zahanati 6). Baada ya uongozi wa Serikali ya Awamu ya 6 tumekuwa ongezeko la hadi kufikia Vituo vya kutolea huduma za Afya 14 (Vituo cha Afya 3 na Zahanati 3). Kutokana na fedha hizo Halmashauri imefanikiwa kupata mafanikio kama ifuatavyo:-

i. Ujenzi wa jengo la Mama na Mtoto na Jengo la dharura ambayo hapo hadi kufikia mwaka 2021 hayakuwepo.



*Jengo la mama na mtoto Hospitali ya Mji Babati, 2022 shilingi 528,480,000.00*



*Jengo la Wagonjwa wa Dharura Shilingi 380,000,000.00*

ii. Vile vile fedha shilingi **1,400,000,000.00** zimepokelewa katika mwaka wa fedha 2023/2024 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu mipya ya kutolea huduma katika Hospitali ya Mji wa Babati.

iii. Ujenzi wa Vituo 4 vya Afya katika Kata za Mutuka, Maisaka, na Sigino kwa gharama ya shilingi 1,280,000,000.00



*Kituo cha Afya Sigino Shilingi 320,000,000.00*

iv. Ujenzi wa Nyumba moja ya familia tatu (3:1) katika Kituo cha Afya cha Mutuka kwa gharama ya shilingi 90,000,000.00






***Nyumba ya mtumishi Kituo cha Afya Mutuka - 2022***

v. Ukamilishaji wa ujenzi wa Zahanati 3 za Imbilili, Chemchem na Singe kwa gharama ya shilingi 379,400,000.00




*Jengo la Zahanati ya Singe, 2021 shilingi 126,000,000.00*

vi. Kuongezeka kwa upatikanaji wa Dawa na Vifaa Tiba kutoka 92% mwaka 2021 hadi kufikia **99.2%** mwaka 2023.



***Duka la Dawa Hospitali ya Mji Babati***

vii. Kuongezeka kwa vitendea kazi kwa kupatiwa magari 2 likiwemo la wagonjwa (ambulance) na gari la usimamizi wa shuhguli za afya




Ambulance na gari la usimamizi

**‵′Kuboreshwa kwa huduma hizi kumewezesha kuimarika wa afya ya jamii na kupunguza vifo visivyo vya lazima hususan mama na Mtoto ambapo kwa sasa wengi wanajifungulia Vituoni na kupata huduma stahiki′′.**

## 2.3 Sekta ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi

***Ibara ya 144 ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM (2020)***

***"Katika Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2015 iliielekeza SMZ kuongeza uzalishaji wa mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi, kusimamia matumizi endelevu ya maliasili, kuimarisha viwanda, biashara, mawasiliano, usafirishaji na utalii kwa lengo la kukuza Uchumi."***

i. Kuongezeka kwa upatikananaji na matumizi ya Mbolea za Viwandani kutokana na kuwepo kwa Programu ya Mfumo wa Ruzuku ya Serikali umewezesha jumla ya wakulima 8,100 kusajiliwa kwa kupatiwa namba za utambuzi ili kunufaika na ruzuku Mbolea ambapo jumla ya Tani 581.65 za Mbolea ya kupandia na kukuzia yenye thamani ya Shilingi 814,310,000 imetolewa. Matumizi haya ya mbolea yameongezeka kutoka wastani wa Tani 120 kwa mwaka 2021 hadi Tani 430 kwa mwaka 2023.

ii. **Kupatikana kwa Vitendea kazi kwa Maafisa Ugani Kilimo:** Jumla ya Pikipiki 21 aina ya Boxer – 125 zilitolewa kwa maafisa ugani kilimo 21 ili kuimarisha huduma za ugani na ushauri wa kitaalam kwa wakulima. Mashine na vifaa vya kupima udongo vimetolewa ili kuwezesha upimaji wa Afya ya Udongo kwenye mashamba ya wakulima. Julma ya wakulima 520 wamenufaika.



*Pikipiki 21 zilitolewa kwa maafisa ugani kilimo 21 mwaka 2023*

iii. **Uimara wa masoko ya mazao ya Kilimo:** Wakulima wamenufaika na uwepo wa **masoko ya Zao la Mahindi na Mbaazi. Zao la Mahindi limeuzwa** kupitia Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (**NFRA)** ambapo Tani 17,000 za mahindi zilinunuliwa na Serikali katika Kituo hicho kilichopo Babati Mjini.



***Picha:*** *Ghala la chakula (NFRA)*

iv. Vile vile zao la Mbaazi limeuzwa kwa bei ya soko ya wastani wa shilingi 2,100 kwa kilo kutokana na kuanzishwa kwa mfumo wa stakabadhi ghalani mwaka 2023 ikilinganishwa na wastani wa shilingi 1,000 kwa kilo kabla ya kuanzishwa kwa mfumo huo.

v. Kuongezeka kwa mafisa ugani kilimo kutoka 21 mwaka 2021 hadi kufikia 27 kwa mwaka 2023.

vi. Aidha, katika Sekta ya Mifugo na Uvuvi, Ujenzi wa majosho matatu ya kuogeshea mifugo katika Kata za Maisaka, Mutuka na Sigino yaliyogharimu kiasi cha shilingi 65,873,843.00



*Josho lililopo kata ya Maisaka kijiji cha kiongozi, 2022.*

vii. Ukarabati wa maabara ya kutolea huduma za mifugo na ujenzi wa josho kwa ajili ya wanyama wadogo katika Kituo cha wakulima na wafugaji Kata ya Nangara ambapo kiasi cha shilingi 17,275,985.00 zilitumika.

## 2.4 Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi

***Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu 2020, katika Ibara ya 229 inaelezea Chama Cha Mapinduzi kitahakikisha Serikali inajenga jamii iliyoelimika, kujiamini na inayomudu kupata mahitaji ya msingi na kuchangia ipasavyo katika ajenda ya maendeleo, ili kufikia azma ya kuwa na jamii na Taifa linalojitegemea.***

i. Katika kipindi cha miaka 3, wananchi wameendelea kunufaika na mikopo ya asilimia 10 inayotolewa na Halmashauri kupitia mapato ya ndani ambapo kiasi cha Shilingi **453,992,628.07** zimetolewa kwa Vikundi 72 ambapo Vikundi 25 vya Wanawake, Vikundi 34 vya Vijana na Vikundi 13 vya Watu wenye ulemavu.





***Picha:*** *Vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu wenye ulemavu wakipewa elimu juu ya mikopo ya 10% kabla ya kukopeshwa.*



Kikundi cha Kiuchumi cha Vijana - Kalakasai

ii. Aidha, kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) umewezesha kutoa fedha kiasi cha shilingi **1,255,371,151** kwa walengwa 2,880 kwa kipindi cha miaka 3. Halmashauri imefanikiwa kuongeza idadi ya

Vijij/Mitaa vilivyopo kwenye Mpango kutoka Vijiji 13 na Mitaa 11 mwaka 2021 hadi kufikia Vijiji 13 na Mitaa 14 mwaka 2023. Vile vile Kaya za wanufaika zimeongezeka kutoka Kaya 1,047 hadi Kaya 2,880 na kiasi cha fedha kimeongezeka kutoka shilingi 111,174,300/= mwaka 2021 hadi kufikia shilingi 1,144,196,851 kwa mwaka 2023 kwa kila dirisha la malipo linapofunguliwa.



*Walengwa wa TASAF wakifundishwa namna ya kuandaa mpango biashara katika kata ya Nakwa, Februari, 2024*



*Walengwa wa TASAF baada ya kufuzu kuandaa mpango biashara katika kata ya Nangara, Feb 2024*

iii. Vilevile kupitia Mpango wa kunusuru Kaya maskini (TASAF), walengwa wameweza kuboresha maisha yao kwa kupata milo 3 kwa siku, kuweza kuwanunulia watoto vifaa vya Shule, kuboresha makazi yao na kuanzisha miradi midogomidogo ya Kilimo, Mifugo na Biashara.



*Mradi wa Barabara ya Nyawari Kata ya Singe ukitekelezwa na walengwa wa TASAF Feb,2024*

iv. Halmashauri imeendelea kuimarisha mazingira ya uwekezaji ambapo kiasi cha **shilingi 891,482,024.00** kimetumika katika uwezaji kwenye maeneo mbalimbali ikiwemo uwanja wa michezo wa Tanzanite Kwaraa



Uwanja wa Tanzanite Kwaraa, 2023

v. Serikali imeendelea kutambua na kuboresha huduma za wajasiriamali wadogo (Machinga) na Maafisa usafirishaji kwa kuwatengea maeneo maalum ya bishara pamoja na kuwajengea Ofisi katika Mtaa wa Maisaka B.



Ofisi ya Machinga na Maafisa usafirishaji Mtaa wa Maisaka "B" Babati Mjini, 2024

## 2.5 Sekta ya Usafi na Udhibiti wa Taka ngumu

Halmashauri imeendelea kutoa Elimu kwa Wananchi kuhusu utunzaji wa mazingira hivyo kupelekea ongezeko kubwa la wananchi katika kaya na wafanyabiashara katika maeneo ya biashara kuwa na vyombo vya kudumu vya kuhifadhia taka, Wananchi wamejenga utamaduni wa kufanya usafi kila wakati ikiwemo kuepuka kutupa taka ovyo kwenye maeneo yasiyo rasmi na kutii Sheria za Usafi wa Mazingira pasipo shuruti.

Vile vile Halmashauri imepata mafanikio mbalimbali ikiwemo:-

i. Kufanyika zoezi endelevu la ukusanyaji wa taka ambapo kwa kipindi cha miaka miwili taka zilizozalishwa ni Tani 26,622 na zilizo kusanywa ni Tani 20,563 hii ni sawa na asilimia 77.2 % ya uzoaji taka.







*Gari la kubeba Taka* *Gari la kunyonya Maji taka*

ii. Kuwa na vifaa vya usafi kama vile uwepo wa Mapipa (Dustbin), Mafagio, Reki na vinginevyo.




*Pipa la Kuhifadhi taka*

iii. Halmashauri inaendelea na uboreshaji wa mazingira ya Ziwa Babati kwa kuanza zoezi la kusafisha ziwa Babati kwa kuondoa Magugu Maji ambapo inatarajia kuwa mazalia ya Samaki yataongekeza na utalii wa ziwa utaongezeka hivyo kuwaletelea kipato wananchi na Halmashauri Kiujumla.



*Sehemu ya Ziwa Babati baada ya kusafisha magugu maji*

## 2.6 Sekta ya Tehama

Kuongezeka kwa matumizi ya Mifumo imara ya TEHAMA kumewezesha kuongezeka kwa uwajibikaji na uwazi katika utoaji wa huduma kwa jamii katika nyanja za Huduma za Afya, Elimu, Kilimo, Fedha, Ununuzi, Utumishi, TASAF, Maendeleo ya Jamii na Mawasilino Serikalini.

## 2.7 Utumishi na Utawala Bora

i. Kipindi cha Miaka 3 cha uongozi wa **Mheshimiwa Dkt.Samia Suluhu Hassan**, **Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,** Halmashauri imefanikiwa kupandisha vyeo watumishi 905 , kulipa malimbikizo ya madeni kwa watumishi 400 ambapo kiasi cha shilingi 1,500,000,000.00 kimetumika. na kuajiri watumishi 112 wapya.

   Hali hii imesaidia kuboresha utoaji huduma kwa wananchi katika maeneo mbalimbali ya Halmashauri ya Mji wa Babati.

ii. Serikali ya Awamu ya sita imefanikisha motisha kwa viongozi kwa kuwalipa moja kwa moja stahiki zao katika Halmashauri ya Mji wa Babati kupitia fedha za ruzuku ya matumizi mengineyo za kila mwezi.

iii. Aidha, imetupatia vitendea kazi mbalimbali ikiwemo Magari 5






*Upatikanaji wa Vitendea Kazi, 2022 - 2024*

**3.7 Barabara za Vijijini na Mijini - TARURA**

Katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Sita, Halmashauri ya Mji Babati imepokea kiasi cha **shilingi 4,065,680,000.00** ambazo zimewezesha utekelezaji wa miradi mbalimbali ya barabara kwa kujenga kilometa 2.4 za lami, kilometa 31 za changarawe, box culvert/madaraja 10 na pipe kalvati line 42.



*Box culvert lililopo barabara ya Babati – Mutuka*



*Daraja barabara ya Nakwa, 2022*

**Taa za barabarani**

Kuimarishwa kwa usalama wa wananchi kwa kuwekwa kwa taa za barabarani ambazo hazikuwepo kufikia mwaka 2021



Taa za barabarani, 2023

### 3.8 Huduma ya Maji vijijini na mjini - BAWASA

Katika kipindi cha mwaka 2021 hadi Desemba, 2023, Mji wa Babati umepokea kiasi cha **shilingi 19,257,447,055.36** kupitia Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Mjini Babati kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi miwili ya:

i. Usambazaji maji katika maeneo ya Dareda – Singu – Sigino na Bagara shilingi 17,663,982,655.36



Mtaro wa Maji kuanzia eneo la plant Kijiji cha Singu, Kuelekea Kata ya Sigino

ii. Ujenzi wa mabwawa ya kuchakata majitaka katika eneo la Maisaka Katani kiasi cha shilingi 1,593,464,400.00



*Picha: Nyumba kwaajili ya muunganiko wa mabomba (Pump House) Kijiji cha Singu*

Usambazaji wa maji katika maeneo tajwa hapo juu, umewezesha kuongezeka kwa kiwango cha upatikanaji wa maji safi na salama katika Mji wa Babati kutoka kiwango cha asilimia 93.8 mwaka 2021 na kufikia asilimia 95 mwaka 2023.



*Picha: Sehemu ya kuchujia Maji (Sedimentation) Kituo cha Singu.*




Tank la Mradi wa usambazaji maji Babati Mjini, 2023




Picha: Tanki la Maji kijiji cha Singu, 2023

## 3 HITIMISHO

Wananchi wa Halmashauri ya Mji wa Babati, wanamshukuru kwa dhati **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** kwa kiasi kikubwa cha fedha za miradi zinazoletwa katika Halmashauri yetu. Vilevile, tunamshukuru Mheshimiwa Rais kwa kusikiliza na kutatua kero za Wananchi na kuongoza Viongozi wa ngazi zote wakiwemo Waheshimiwa Mawaziri, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Wabunge na Madiwani kwa kuendelea kutatua changamoto za wananchi kwa kuwafikishia miradi ya maendeleo. Hivyo "**SERIKALI IMEAWASIKIA NA IMEWAFIKIA WANANCHI.** Tunamuahidi kuzisimamia kwa weledi na uadilifu na kufanya matumizi yenye tija ili kuhakikisha kwamba malengo yaliyowekwa na Serikali katika kuwapelekea huduma bora Wananchi yanafikiwa na hatimaye kuboresha maisha ya wananchi.

**"JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA."**